Kuna kipimo ndani ya fikra zako ambacho ndio kinaamua unastahili kuwa mmiliki juu ya kiasi gani cha fedha.

Naweza kusema kuna kiasi cha fedha kinachopatikana ndani ya fikra zako ambacho ndio kinatumika kuita fedha zilizo nje yako.

Fedha iliyo ndani yako ndio itakayoita fedha zilizo nje yako.

Fedha haiwezi kukufahamu kama hauna fedha ndani yako. Fedha iliyondani yako ndio utambulisho wa fedha zilizo nje yako.

Hivyo ni ngumu kupata fedha kwa nje ikiwa hauna fedha kwa ndani.

Fedha ili zije kwako ni lazima zione ndani yako kuna wenzao.

Mfano leo wengi tunatumia simu zenye finger print, au zinazotumia voice lock.

Unapotaka kuanza kutumia fingerprint kwenye simu yako, ili kuifunga na kuifungua kupitia alama za kidole chako, ni lazima ujaze taalifa kwenye simu yako kwa kuweka kidole chako kwa mara ya kwanza.

Ukiweka kidole kwa mara ya kwanza taarifa zako zinahifadhiwa kwenye mfumo wa simu yako.

Na baadaye akija kuweka mtu mwingine kidole ile simu itagoma kufunguka kwa sababu taarifa ya kidole hicho hakipo kwenye hiyo simu.

Na kidole pekee kinachoweza kufungua hiyo simu ni kile tu

ambacho kiliweka taarifa zake kwenye simu hiyo kwa mara ya kwanza.

Kwa maana kwamba simu yako itatafuta taarifa zinazoendana na zile zilizowekwa mara ya kwanza na kama taarifa zinafanana ndipo kifaa kitakubari kufunguka.

Taarifa za ndani ya simu zinatafuta taarifa za nje ya simu ambazo zinafanana ili simu ifunguke.

Ndivyo ilivyo hata kwa fedha, fedha iliyo nje yako itakuja kulingana na fedha iliyondani yako kwa sababu zinafanana.

Fedha zilizo nje hazina shida shida ni taarifa za fedha ulizonazo ndani yako.

Kilicho ndani kinavuta kilicho nje.

Iko hivi kama hakuna upendo ndani yako ni ngumu kuona upendo wa wengine.

Ukiwa umekasirika hata ukiona watu wanafurahi utaona wanakukera na huwenda wanakukejeli lakini kumbe hapana wao wanamambo yao tu huko.

Hivyo elewa huwezi kupokea kwa wingi kitu ambacho haunacho ndani yako.

Ukiwa na huzuni ni kazi ngumu sana kupokea furaha ya watu wengine, wakati mwingine ukiwa na furaha ni ngumu kupokea huzuni ya watu wengine.

Kabla hujashika milioni tano hakikisha ndani yako unafikra zenye thamani ya uwezo wa kubeba hiyo milioni tano.

Kuna kiasi cha fedha ukiwa nacho hata hofu inazidi. Wakati mwingine unaweza ukawa unajihisi kwamba kila mtu huwenda anajua umebeba kiasi hicho cha fedha.

Hicho kiasi cha fedha ni kikubwa kuliko kiwango unachoweza kukimiliki ndani yako.

Labda tuchukulie umepewa maji na soda ya 7 up katika glass mbili tofauti.

Mwanzoni kwa kuangalia unaweza ukashidwa kutambua ipi ni soda na yapi ni maji.

Unapoonja ndipo utakapoweza kutofautisha.

Unajua kwanini umeweza kutofautisha? Ni kwa sababu tayari

ubongo wako unataarifa kuhusu ladha ya maji.

Hivyo taarifa zilizotunzwa mara ya kwanza kwenye fikra zako kuhusu maji zinajulikana, hivyo unafikia hitimisho kwamba hayo uliyokunywa si maji halisi hata kama yanafanana muonekano na maji.

Ndivyo ilivyo hata kwa fedha haijalishi utapokea mikononi mwako fedha kiasi gani, hiyo fedha itapimwa kwenye vipimo vya fedha ya kwenye fikra zako.

Hivyo unapaswa kupalilia kwanza fikra zako ili uweze kuwa na uwezo wa kumiliki fedha kwa viwango vikubwa.

Huu ni mchakato wa siku kwa siku na wa vitendo.

Elewa hapa kwamba huwezi kufanikiwa kifedha nje hadi ueweza kufanikiwa kifedha ndani.

Tajiri aliyefirisika ni vyepesi kuwa tajiri tena kuliko masikini aliyekuwa masikini siku zote.

Unachokitafuta hakikisha kimo tayari ndani yako.

Fedha hufuata fedha, mafanikio yanavutia mafanikio. Ukuu unavutia ukuu.

Huna haja ya kuwaza hali uliyonayo sasa ila unapaswa kulisha fikra zako taarifa ya kule unataka kuwa, na baadaye fikra zako zitakuinua kufikia hapo unapotaka kufikia.

Fikra zako ni chombo ambacho kinakupeleka kule unapokipa taarifa kikupeleke.

So uelewe kwamba sumaku ya fedha unazozitaka ni zile fedha ulizonazo kwenye fikra zako.

Tengeneza fikra zako katika umbo la kile unataka uwe nacho au ukimiliki.

Sio wewe unayevutia fedha ila ni fedha ndani yako ndio zinavuta wenzao.

Umewahi kusikia watu wakisema kwamba mtaji wa biashara sio fedha ila ni wazo na mtazamo wako?

Nazani hapa ndio utanielewa vizuri.

Ni kwamba hatuanzi na mtaji fedha kama hayo makaratasi, ila tunaanza na mtaji fedha zilizo ndani ya fikra za muhusika.

Sikia, ndege wa rangi moja huruka pamoja, na vitu vitakuja kwako kulingana na vile vilivyo ndani yako.

Ndio maana tunasema mafanikio sio vile ulivyonavyo ila vile ulivyo au vile ulivyo ndani yako.

Siri ya mafanikio kifedha ni zaidi ya kuwa na makaratasi yanayoitwa fedha.

Mafanikio kifedha ni kuwa na hazina ya fikra yenye ufahamu fedha ndani yake.

Ni muhimu kuchukua muda wako kutafakari (**meditation and imagination**) juu ya viwango unavyotaka kufikia kiuchumi.

Tunatenga muda kutafakari ili kujenga ndani yetu kile tunachotaka kitokee nje yetu.

Kutafakari ni kulisha fikra zako chakula (taarifa) chenye nguvu

kinachoweza kuchochea kwa haraka matokeo unayoyataka nje yako.

Unapaswa kuwa tajiri ndani yako kwanza ndipo utajiri nje yako utakapojionyesha.

Unapaswa kuwa na fedha ndani yako kwanza ndipo utafanikiwa kuwa na fedha za kutosha nje yako.